# TAWJA kuyapa elimu ya sheria makundi maalum

**NA ASYA HASSAN**

CHAMA cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA) kimeendelea na mpango wake wa kutoa elimu ya kisheria kwa makundi mbali mbali hasa yanayojihusisha na harakati za kusaidia wananchi katika masuala ya haki.

Ofisa Mradi wa chama hicho, Asha Hassan Komba, alisema hayo alipokuwa katika mafunzo ya kisheria ya kuwajengea uwezo Wanaharakati, Masheha, Wasaidizi wa Sheria na Maofisa wa madawati ya jinsia wa mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja

Alisema licha ya juhudi za serikali na wadau mbalimbali katika kuelimisha jamii kuhusu masuala ya kisheria, bado kuna upungufu wa uelewa na mwamko, hali inayosababisha watu wengi kukosa haki zao, ikiwemo umiliki wa ardhi, mirathi na kupambana na ukatili wa kijinsia.

Akizungumzia lengo la programu hiyo, Mratibu wa chama hicho kanda ya Unguja, ambaye pia ni Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Sara Omar Hafidhi, alisema kuwa TAWJA inalenga kufikisha elimu ya kisheria hadi ngazi ya jamii kwa kutumia njia mbalimbali, ikiwemo kutoa mafunzo katika masoko, skuli, vituo vya daladala na maeneo mengine ya mikusanyiko.

Alisema hatua hiyo pamoja na mambo mengine itasaidia kuongeza uelewa na mwamko wa jamii kudai haki zao.

"Ni muhimu kwa jamii kubadilika na kuondokana na muhali katika kudai haki zao, malezi ya pamoja na elimu sahihi vitasaidia kuleta kizazi bora na chenye uelewa mpana wa masuala ya kisheria", alisema Sara.

Nao washiriki wa mafunzo haya walieleza kufurahishwa na hatua hiyo na kuahidi kutumia maarifa waliyopata kwa kuisaidia jamii kuelewa haki zao na kushiriki katika kuzidai kwa njia sahihi.

Mafunzo haya yaliyoandaliwa kwa kushirikiana na UN WOMEN yalihusisha mada kuhusu udhalilishaji, sheria za watoto, mirathi, wosia, nafasi ya wanawake katika uchumi na masuala mengine muhimu ya kisheria.

Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania kilianzishwa mwaka 2000, na kwa kipindi cha miaka 25 sasa, kimeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuelimisha jamii kuhusu haki zao za msingi.

Mafunzo kama haya yatatolewa Unguja na Pemba, yakitarajiwa kuleta mabadiliko chanya katika uelewa wa sheria miongoni mwa wananchi.

# Watendaji manispaa waridhishwa utatuzi changamoto za usafiri

**NA HAFSA GOLO**

WATENDAJI wa Divisheni wa Mipango Miji na Usimamizi wa Taka wa Baraza la Manispaa Mjini wamesema wameridhishwa na utendaji, ufatiliaji wa karibu na utatuzi wa changamoto zilizokuwa zikilikabili baraza hilo.

Walisema tangu kuingia kwa Mkurugenzi mpya wa Baraza la Manispaa ya Mjini, Hasna Attai Masoud, yapo mabadiliko makubwa ya kiutendaji kutokana na juhudi zake za kutatua matatizo ya usimamizi wa taka na kuyapatia ufumbuzi unaofaa kwa wakati.

Walisema hatua hiyo imewaridhisha watendaji hao kwani imeongeza ufanisi,uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu jambo ambalo limechangia kupunguza malalamiko kwa wananchi.

Naye Msimamizi wa taka na usafi wa baraza hilo, Ikrima Jumanne Khamis, alitaja miongoni mwa changamoto alizozisawazisha ni kuyafanyia marekebisho magari ya taka yaliyokuwa yakiharibika mara kwa mara kutokana na uchakavu wa magari hayo.

"Hizi gari zimefanyiwa matengenezo na zinafanya kazi vizuri na kuwezesha kuondoshwa taka katika manjaa kwa wakati", alisema.

Pamoja na mafanikio hayo aliiomba serikali kuwafanyia utaratibu wa kuwapatia magari mapya ya taka ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

Alifahamisha kuwa eneo jengine lililopatiwa ufumbuzi ni pamoja na kuongeza nguvu kazi katika usimamizi wa taka,rasilimali watu katika uzoaji na uondoshaji wa taka katika maeneo ya manispaa ya mjini.

Kwa upande wake Mhandisi Aminia Juma Ali, alisema kwamba moja ya changamoto inayowakabili ni uhaba wa wakaguzi wa maeneo ya manispaa katika masuala ya ujenzi.

"Tunaamini kutokana na juhudi za kiongozi huyo changamoto hii inaotokana na watendaji wengi kustaafu kwa kushirikiana na watu wa utumishi itapatiwa ufumbuzi", alisema.

Wakizungumzza na Zanzibar Leo, baadhi ya wananchi wanaoishi maeneo ambayo awali yalikuwa na mrundikano wa taka na kulalamika juu ya kuhofia usalama wa afya zao walisema kuwa taka hivi sasa zinaondoshwa kwa wakati.

Mkaazi wa Mwantenga kwa Mabata, Hamid Ameir, alisema kuwa kipindi hichi taka zimekuwa zikiondoshwa kwa muda muwafaka.

"Sijui wamesemwa na wakubwa wao au ndio uchaguzi unakaribia wanataka kura, ilimradi tunashkuru tu kwa kuondoshwa taka mapema kabla hazijaanza kuzagaa na kuwa kero kwetu", alisema.

Naye Fatma Ali Khamis, mkaazi wa Magogoni, alikiri kuwepo kwa juhudi za uondoshaji taka upo vizuri kwa sasa jambo ambalo limesaidia kuimarisha mazingira katika eneo hilo.

"Ndugu mwandishi umetusaidia sana hivi sasa taka zinaondoshwa kwa wakati naomba usichoke kufatilia suala hili ili waendelee kutuondoshea taka kwa wakati", alisema.




*MWENYEKITI w Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Goerge Joseph Kazi, akikunjua kitambaa kuashiria kuweka jiwe la msingi jengo la ofisi ya tume hiyo wilaya ya magharibi 'B' linaloendelea na ujenzi wake huko Mazizini. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo Jaji Aziza Iddi Suwedi. (PICHA NA FAUZIA MUSSA)*

# 'Tumieni teknolojia kuvuna maji kwa matumizi ya kilimo'

**NA SALAMA MOHAMMED, WKUMM**

AFISA Mradi wa Haki ya Kupata maji na Uvunaji wa Maji wa gharama nafuu kwa wakulima wadogo, Mohamed Yussuf Haji, amewataka wakulima waongeze jitihada ya kuvuna maji ili kuimarisha shughuli zao.

Haji ambaye anatoka katika Jumuiya ya ukulima wa mboga na matunda amesema kufanya hivyo pia kutainua kilimo nchini na wakulima kupata mazao ya kutosha na kujiongezea kipato.

Aliyasema hayo jana katika Ofisi za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Maruhubi alipokua akizungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusiana na hatua zinazochukuliwa katika mradi huo kwa wakulima wa Unguja.

Alisema lengo la mradi huo ni kuongeza ustahamilivu wa uhaba wa maji unaotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi miongoni mwa familia za wakulima wadogo katika wilaya zenye mazingira magumu kupitia ushawishi wa matumizi ya teknolojia maalum za uvunaji maji kwa gharama nafuu.

Alieleza kuwa mradi huo ili ufanikiwe ni lazima uwe na teknolojia ya uvunaji maji zilizobuniwa na wakulima wenyewe sambamba na uwepo wa teknolojia za ndani za wakulima hao zilizounganishwa katika mipango ya kukabiliana na hali ya hewa.

Sambamba na hayo alifahamisha kuwa kwa sasa baadhi ya wakulima wadogo wameanza kuhamasika na kufaidika na uvunaji huo wa maji hivyo aliwaomba wakulima wengi zaidi kujitokeza na kutumia mbinu hizo wapate kunufaika.

Naye mkulima kutoka Sheria ya Mgeni Haji, wilaya ya Kati Unguja, Shaabani Pandu Haji, aliwashauri wakulima wenzake kutumia vyema mvua zinaponyesha na kuihifadhi maji pindi zinapokatika ili kuwa na muendelezo nzuri wa kilimo chao.

Shaabani alisema amepiga hatua nzuri kwenye kilimo cha mazao ya mboga kama mabilingani na pilipili kupitia nadharia ya uvunaji maji nab kupata tija lakini kutokana na miche yake kuliwa na wadudu waharibifu ameomba kupatiwa dawa za kilimo hai za kuulia wadudu hao ili kuzidi kuendelea kuimarisha kilimo chake.

Mradi huo wa miaka mitatu unatarajiwa kuwanufaisha wakulima 400 waliopo katika vikundi 20 vilivyopo wilaya za Kaskazini 'A', Kusini, Kati na Magharibi 'A' Unguja, unaofadhiliwa na Shirika la Organic Denmark unatekelezwa Uganda, Tanzania bara na Zanzibar (Unguja tu), utagharimu shilingi 144,085,095 utakapokamilika.

PDF Scanner ACE Scanner